

TANGAZO LA SERIKALI Na. 31 la tarehe 12/1/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (USAFI WA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI
YA WILAYA YA ROMBO YA MWAKA 2023

Jina
TS Na.
162 la 2019

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ya Mwaka 2023 na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ya Mwaka 2019 ambayo hapa imerejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Kufutwa na
kuandikwa
upya kwa
aya ya 24

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 24 kama ifuatavyo:

“Ada ya uzoaji wa taka 24.-(1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji wa taka kutoka kila kaya au kwa mtu yeyote mwenye shughuli ya biashara au mzalishaji taka wa aina yoyote kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada ya uzoaji wa taka italipwa kila tarehe 28 ya kila mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejesta ya wazalishaji taka.

(3) Endapo mzalishaji taka atakuwa hajalipa ada ya mwezi kufikia tarehe 5 ya mwezi unaofuatia atakuwa ametenda kosa.

(4) Iwapo mzalishaji taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo, Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kudai deni la ada na kumfikisha mahakamani.”.

Marekebisho ya aya ya 26

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 26 kwa kuongeza aya ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

“(2) Halmashauri itatenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutupa taka yatakayojulikana kama dampo au ghuba ambapo watu hawataruhusiwa kujenga au kuishi karibu na maeneo hayo.”.

Marekebisho ya aya ya 28

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 28 kwa kuongeza mara baada ya aya (g) aya mpya kama ifuatavyo:

“(h) atamhamasisha au kumshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ada za uzoaji taka chini ya Sheria Ndogo hii;

(i) atadharau au atashindwa au atakwepa kulipa ada au kutekeleza agizo alilopewa chini ya Sheria Ndogo hii;

(j) atakataa kufanya usafi kwenye eneo lake siku iliyopangwa na Halmashauri.”.

Kufutwa na kuandikwa upya kwa Jedwali la Kwanza

5. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya Jedwali la Kwanza kama ifuatavyo:

*Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya
Wilaya ya Rombo*

Tangazo la Serikali Na.31 (Linaendelea.)

“ _____

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 7(2))

ADA ZA HUDUMA ZA USAFI NA UZOAJI WA TAKA

Namba	Eneo	Ada kwa mwezi (Shilingi)
1.	Nyumba za kuishi kila kaya (maeneo ya mijini au ya kibiashara)	3,000/=
2.	Maduka ya rejareja	5,000/=
3.	Mashine ya kukamua mafuta ya alizeti	5,000/=
4	Maduka ya jumla ya bidhaa na chakula	5,000/=
5	Migahawa	5,000/=
6	Mashine za kukoboa au kusaga	10,000/=
7	Vilabu vya pombe za kienyeji, baa, grocery,	5,000/=
8	Mama lishe au Baba lishe au Nyama choma au chipsi inayojitegemea	5,000/=
9	Viwanda vya useremala na mashine za mbao	10,000/=
10	Bucha (Maduka ya Nyama au samaki)	5,000/=
11	Nyumba za kulala wageni	5,000/=
12	Saluni (Ususi au Vinyozi)	3,000/=
13	Gereji	5,000/=
14	Ghala	7,000/=
15	Kituo cha kuuza mafuta	10,000/=
16	Ofisi za Taasisi mbalimbali	5,000/=
17	Hoteli	10,000/=
18	Stoo za mkaa	5,000/=
19	Mafundi kushona nguo	3,000/=
20	Mafundi vyuma(wahunzi)	10,000/=
21	Kumbi za starehe au sinema	10,000/=
22	Maeneo ya kuoshea magari au pikipiki	5,000/=
23	Zahanati au kituo cha afya au hospitali	20,000/=

Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo

Tangazo la Serikali Na.31 (Linaendelea.)

24	Majengo mengine yasiyotajwa	20,000/=
25	Viwanda vikubwa	30,000/=
26	Viwanda vya kati	25,000/=
27	Viwanda vidogo	15,000/=
28	Kutupa uchafu katika eneo la dampo	10,000/= kwa kila tripu

*Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya
Wilaya ya Rombo*

Tangazo la Serikali Na.31 (Linaendelea.)

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 3/3/2023 na Lakiri imebandikwa mbele ya:-

GODWIN JUSTIN CHACHA,
*Mkurugenzi Mkuu,
Halmashauri ya wilaya,
Rombo*

*Gilbert Alex Tarimo,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya wilaya,
Rombo*



Dodoma,
....., 2023

NAKUBALI,

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb.),
Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI,